# Vunja UKIMYA Ondoa VIKWAZO!

## Unawezaje kufanya Elimu kuwa Salama kwa Wasichana?

**Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia**

**Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Unyanyasaji wa Kijinsia Mwaka 2016**

**Mapitio ya Kampeni**

GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism

### *Kauli Mbiu: Vunja Ukimya, Ondoa Vikwazo! Unawezaje Kufanya Elimu Kuwa Salama kwa Wasichana?*

Mwaka huu tunaadhimisha miaka 25 ya kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati dhidi ya Unyanyasaji wa Kijinsia ikiratibiwa na Kituo cha Uongozi wa Wanawake Duniani. Kwa sababu ya harakati zilizofanywa na kituo hiki, kampeni sasa imesambaa duniani kote. Katika ngazi ya kanda wanachama wa mtandao wa kuzuia ukatili wa kijinsia wamekuwa wakishiriki katika kampeni tangu mwaka 2004. Mwaka huu kampeni ya kimataifa inalenga katika kuchambua uhusiano kati ya matumizi ya kijeshi na haki ya kupata elimu katika maeneo yenye migogoro na vita, katika maeneo yenye amani, na mazingira mbalimbali ya elimu. kampeni itaweza kuonyesha uhusianao wake kati ya ukatili wa kijinsia na matumizi ya kijeshi, yanavyoambatana na mfumo dume wenye ubaguzi na kujikita na uhusiano wake na matumizi ya mamlaka.

Katika kuhusisha kampeni ya kikanda na kimataifa, kauli mbiu ya Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia inalenga kufanya elimu kuwa salama kwa wote, hasa wasichana na wanawake vijana, kwa kuainisha miundo ya ubaguzi kwa wanawake na wasichana katika mfumo wa elimu kuanzia majumbani, jamii, na mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na sera za serikali na mifumo inayoathari wasichana shuleni. Kampeni itachambua jinsi ubaguzi na matukio mengine katika mfumo wa elimu yanayosababisha wasichana na wanawake kufanyiwa ukatili. Itajikita katika jitihada za kimataifa ili kuhakikisha elimu bora ambayo ni shrikishi na yenye usawa kama ilivyoainishwa katika Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu

Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni tatizo katika sehemu nyingi za dunia na sasa linashughulikiwa kimataifa kama tatizo la afya ya jamii, sera za kijamii na ni ukuikwaji wa haki za binadamu. Inakadiriwa kuwa duniani kote asilimia 30% ya wanawake duniani kote hufanyiwa ukatili wa kimwili au wa kingono na wenzi wao, asilimia 7% ya wanawake duniani kote hufanyiwa unyanyasaji wa kingono na watu wasio wenzi wao. Takribani wasichana na wanawake milioni 100-140 wamefanyiwa ukeketaji wa wanawake (FGM) na milioni 70 wameolewa kabla ya umri wa miaka 18. Kulingana na makadirio ya UIS, watoto milioni 24 kamwe hawatahudhuria darasani. Nusu ya watoto wote walio nje ya shule Kusini mwa jangwa la Sahara hawataandikishwa shule.

Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni kiini cha kutokuwepo na usawa wa kijinsia. Kihistoria na mpaka sasa wasichana na wanawake wana hadhi ya chini katika jamii. Mamlaka ambayo wanaume wanayo na wanayopewa yanatokana na mitazamo, tabia na matarajio ambayo wanawake na wanaume hujifunza kama wanajamii. Kama watoto wadogo, majukumu yao ya kijamii (pia huitwa majukumu ya kijinsia) mtu huweza kujifunza, (k.v. jinsi jamii yetu inavyoamini wasichana na wavulana, wanawake na wanaume wanavyopaswa kutenda) na hii ina athari hasi kubwa juu ya uchaguzi, uhuru na maisha ya elimu ya wasichana na wanawake.

Halikadhalika, katika mazingira ya nyumbani, kwa sababu ya majukumu yao kijamii wasichana wanatumia muda zaidi katika kazi zao za nyumbani na muda kidogo katika kujisomea na maandalizi ya masomo. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na shirika la UNICEF wakati wa Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa kike tarehe 11 Oktoba, wasichana walio na umri kati ya miaka 5 na 14 wanatumia asilimia 40 ya muda zaidi, au masaa milioni 160 zaidi kwa siku, katika kazi za nyumbani zisizo na malipo za kuchota maji na kukusanya kuni ikilinganishwa na wavulana wa umri wao. Mara nyingi wasichana huachishwa shule na kuolewa hata kabla hawajafikisha umri wa miaka 18, mara nyingi mambo haya hufanyika kwaajili ya manufaa ya mahari ambayo ndoa hiyo italeta. Wasichana wanapata hasara zaidi katika upatikanaji wa elimu kutokana na mazingira ya shule. Kunauwezekano mkubwa kufanyiwa unyanyasaji, mashambulizi, kutekwa nyara na ubakaji na watu wasiojulikana.

Ndani ya mazingira ya shule, wasichana wanakabiliwa na unyanyasaji na ukatili katika ngazi mbalimbali. Wanaweza kufanyiwa unyanyasaji katika mfumo wa uonevu na unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa wanafunzi wa kiume, walimu na wafanyakazi wengine. Mara nyingi wasichana wanaacha shule kutokana

na vifaa vya kuhudumia mahitaji yao maalum ikiwa ni pamoja na usafi wakati wa hedhi kutokidhi haja. Mbali na ukatili wanaoupata, mafundisho yanayofundishwa shuleni huhamasisha kutokuwepo kwa usawa wa mamlaka kati ya wanawake na wanaume, zaidi ya hayo, mchakato wa mahusiano unahamasisha wanaume na wavulana kuwa na mamlaka juu ya wanawake.

ubaguzi ambao wanawake na wasichana unaowakabili unaambatana na vitendo vya ukatili ambavyo vinasababisha vikwazo katika ushiriki wao  ndani ya jamii na pia vinaathiri maendeleo katika nyumba zao, jamii na shuleni. Linapokuja suala la elimu, wasichana wanakabiliwa na ubaguzi wa kijinsia na ukatili katika suala la upatikanaji wa elimu na usalama katika maeneo ya elimu, na kuchochea wasichana kuwa na hadhi ya chini katika jamii.

Kuna matumaini. Kama tunavyofahamu, wengi wa wavulana na wanaume si wakatili; wanafanya maamuzi ambayo yanadhihirisha imani yao katika usawa, haki na heshima. Vile vile, wanawake wengi hawaruhusu ukatili dhidi ya wanawake. Hata hivyo kwa ujumla, wasichana wengi na wanawake, wavulana na wanaume wapo kimya kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na usawa wa mamlaka unaoliendeleza hilo. Kipindi hiki cha Siku 16 ni wakati ambao watu wote wanaweza kuzungumza na kushughulikia kukosekana kwa usawa na ukiukwaji wa haki dhidi ya wasichana na wanawake.

## Masuala ya Kampeni

Mwaka huu, kampeni ya Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia inalenga katika kuuliza wanajamii, wazazi, shuleni na watunga sera kuhusu upatikanaji wa elimu salama kwa wasichana na wanawake. Tunavunja ukimya kwa kuainisha na kuweka wazi masuala ya ndani ya nyumba zetu, shuleni na katika jamii ambayo yanasababisha vikwazo katika upatikanaji wa elimu kwa wanawake na wasichana na masuala ambayo yanapelekea maeneo ya elimu kutokua salama. Tunapoainisha suala la kufanya elimu kuwa salama kwa wote, mashirika yanaweza kuchagua na kuonyesha moja au mchanganyiko wa masuala yafuatayo yanayosababisha kikwazo katika elimu ya wasichana katika jamii zao na kutoa wito juu ya suala hilo ili hatua ziweze kuchukuliwa.

1. **Upatikanaji wa elimu**- Hakikisha wasichana wote wameandikishwa shuleni na kuendelea na masomo mpaka watakapomaliza elimu ya ngazi ya juu
    a. Je, wasichana na wanawake vijana wanapata fursa ya kwenda shule katika hali ya usawa katika jamii yako
        i. Kuna idadi gani ya wanafunzi wa kike na wa kiume katika ngazi mbalimbali za elimu katika jamii yako? Je uwiano unabadilika katika ngazi ya elimu ya juu? Kwa nini?
        ii. Je, kuna sera zozote ambazo ni za kibaguzi dhidi ya wasichana ( mfano. wasichana kufukuzwa wanapopata mimba, ukosefu wa faragha / usafi wa mazingira kwa wasichana, nk)
    b. Wasichana wanapokwenda shuleni  ni  athari zipi za kiusalama wanazokabiliana nazo katika jamii yako? kwa mfano. unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, utekaji nyara
    c. Hata wakati wasichana wanapopata elimu wanaruhusiwa kumaliza shule? Ni vikwazo gani wanavyokabiliana navyo wasichana vinavyowakwamisha kumaliza shule?
2. **Usalama shuleni** -Fanya mazingira ya shule kuwa salama na mazuri kwa wanawake na wasichana, hakikisha miundo mbinu ya shule inakidhi mahitaji yao maalum
    a. Je, ni vifaa gani vya shule vinavyopatikana (Ni kwa namna gani vinakidhi mahitaji maalum ya wasichana / wanawake vijana?) k.m ni utaratibu gani umewekwa kwa ajili ya kujihifadhi wakati wa hedhi? Kuna vyoo tofauti kwa wasichana na wavulana?
3. **Mfumo wa elimu** – Shinikiza mabadiliko ya mifumo ambayo inasababisha wasichana kufanyiwa ubaguzi hasi na kutokuwepo na usawa wa mamlaka. Hakikisha mitaala na vitabu vya kiada vinahamasisha na kuonyesha usawa wa jinsia.
    a. Ni maudhui gani yanayofundishwa shuleni yanayochochea ubaguzi wa wasichana na wanawake vijana – na baadaye kuwanyima fursa ? (Je maudhui ya elimu yanapanda mbegu za kutokuwa na usawa wa mamlaka? Je inachochea fikra katika nchi ya kuwa wavulana wana thamani zaidi kuliko wasichana?)
    b. Je wasichana na wanawake vijana wanahamasishwa kushiriki kama vijana wenzao wa kiume?
    c. Je, wasichana na wanawake vijana wanafanyiwa unyanyasaji wa kijinsia / ukatili wa kingono kutoka kwa walimu na wanafunzi wengine?

*Siku 16 za Uanaharakati ni fursa kwa ajili ya kuelekeza nguvu katika kuleta mabadiliko chanya. Je, wewe unahusikaje?*

Sustainable development goal 4: Ensure inclusive and equitable quality education and promote lifelong learning opportunities for all. Retrieved from https://sustainabledevelopment.un.org/sdg4

WHO (2013). Global and regional estimates of violence against women: prevalence and health effects of intimate partner violence and non-partner sexual violence. Geneva.